

# MBINU RAHISI ZA UANDISHI WA VITABU

## UTANGULIZI

Uandishi wa vitabu mara nyingi huhusishwa na taaluma ya uandishi wa habari na kujenga dhana kuwa wasio na taaluma ya uandishi wa habari hawawezi kuwa waandishi bora wa vitabu. Kweli ya msingi ni kuwa hivi ni vitu viwili tofauti, ingawa kuna sehemu vinategemeana.

Kila mtu anaweza kuwa mwandishi bora wa vitabu akizingatia tu kanuni muhimu katika uandishi wa kitabu husika na mwana–taaluma ya uandishi wa habari anaweza kutumika kuboresha eneo la uhariri. Mfano; Mchungaji akiandika kitabu

kinachoangazia taaluma yake kinakuwa bora zaidi katika kufikisha ujumbe kwa walengwa .

Uandishi wa vitabu ni hitaji la msingi kwa kila mtu ili kazi au maisha yake yaendelee kuishi hata baada ya mwili na roho yake kufarakana (kufariki dunia).

Karibu mambo yote yanayofanyika duniani, msingi wake ni uandishi. Mshuhudiaji wa Injili atahitimisha ujumbe wake kwa nukuu kutoka katika maandishi. Wakili anayejenga hoja iwe ni kufungua mshtaka mahakamani au kumtetea mshtakiwa atarejea katika vitabu na hata Jaji anapomhukumu mtu iwe ni kifo, kifungo au kumwachia huru hurejea katika nukuu ya vitabu “Imeandikwa” na hapa ndipo tunapouona umuhimu wa kuwa sehemu ya wanaoandika.

Ukipita mahali ukakuta mtu anamshuhudia mwingine kwa habari ya Ujumbe wa Injili utamsikia akisema, “Imeandikwa” anaweza asitumie maneno au lugha hii lakini  lazima atarejea maandiko au nukuu iliyoandikwa kwenye kitabu ili kutoa ushahidi wa ushuhuda au ushuhudiaji wake. Zifuatazo ni mbinu rahisi za kukuwezesha kuwa mwandishi bora wa vitabu:

## 1. UCHAGUZI WA WAZO

Hatua ya kwanza kabisa katika uandishi wa kitabu ni kuchagua mada au wazo bora. Hakikisha unachagua wazo au mada kwa makini ambayo itakuwezesha kukamilisha lengo lako. Unaweza kuzingatia haya:

- **Chagua mada ambayo unaipenda na unaielewa vyema.**
- **Chagua mada ambayo inahitajiwa na wasomaji.**
- **Chagua mada ambayo haikiuki sheria au maadili ya eneo unalolenga.**
- **Chagua mada ambayo inaziba pengo lililoachwa na vitabu vingine.**
- **Chagua mada ambayo una mamlaka ya kuiandika kulingana na uwezo/sifa au taaluma yako.**

## 2. PANGILIA KABLA YA KUANDIKA

Mpangilio ni jambo muhimu katika uandishi wa vitabu. Hakikisha unapangilia mtiririko wa mawazo pamoja na muundo mzima wa kitabu chako kabla ya kuanza kuandika. Hakikisha unabainisha sura zitakazokuwepo kwenye kitabu chako pamoja na maudhui ya sura zote za

kitabu. Ni kama ujenzi wa nyumba, lazima uandae ramani ya nyumba ili uione picha yake kabla ya kujenga. Ikiwa unashindwa kupanga mawazo pamoja na kubainisha sehemu kuu za kitabu chako, basi kuna haja ya kutafakari upya wazo ulilolichagua.

## 3. ZINGATIA KANUNI ZA UANDISHI

Ni jambo la lazima kuzingatia kanuni bora za uandishi kama vile; matumizi bora ya lugha, mpangilio wa hoja au mawazo pamoja na matumizi ya alama za uandishi. Ikiwa sio mtaalamu mzuri wa lugha ni muhimu kumpa mtaalamu wa lugha husika aboreshe kazi yako.

## 4. MAZINGIRA BORA YA UANDISHI

Sio kila mazingira yanafaa kwa ajili ya kufanya kazi ya uandishi; ni lazima uhakikishe unatafuta mazingira ambayo ni tulivu na yasiyokuwa na muingiliano. Katika kuandaa mazingira bora zingatia haya:

- Chagua eneo ambalo ni tulivu na linakupa utulivu wa kiakili.
- Ondoa vitu ambavyo vitakutoa katika kusudi kwa kuipa akili yako taarifa zingine kama vile radio, Tv, simu nk.

## 5. TAFUTA KAZI INAYOSHABIHIANA

Mara nyingi kila kitu duniani kina kitu kingine kinachoshabihiana nacho. Tafuta kitabu ambacho kinakaribiana na kile unachotaka kuandika; kwa kufanya hivi utaweza kukitumia kama mwongozo wako, lakini pia utapanua wazo kutoka alipoishia. Tazama jinsi ambavyo mwandishi wa kitabu husika amepanga mawazo au hoja katika kitabu chake; tazama pia lugha na mbinu nyingine za kiuandishi alizozitumia kukamilisha kazi yake.

Epuka makosa aliyofanya ili kazi yako iwe bora zaidi na unaweza kunukuu mada aliyojadili lakini kwa

kumpa utambulisho wa kazi yake bila kukiuka hakimiliki.

## 6. TAMBUA HADHIRA

Ni jambo la msingi kuzingatia kweli kuwa uandishi hutofautiana baina ya aina moja ya hadhira na nyingine. Uandishi wa vitabu vya watoto ni tofauti na uandishi wa vitabu vya vijana au wazee. Hivyo ni muhimu ukabaini ni kundi gani na lenye sifa gani unalolilenga katika kitabu chako. Ifahamu vyema hadhira yako, fahamu inapendelea nini ili uweze kuilenga vyema.

Ni vyema pia kukielekeza kitabu katika hadhira unayoilenga na kuweka hilo wazi katika kurasa za mwanzo za kitabu. Waandishi wengi hutaja moja kwa moja kundi wanalolenga katika dhana ya uandishi Kitabu pia kinaweza kupewa heshima ya mtu ambaye mwandishi anaamua kukitoa kwake kulingana na mchango flani kwenye maisha yake na

wakati mwingine hata sehemu ya mapato huelekezwa kwa mtu huyo au kundi fulani. Katika dhana hiyo maneno kama "Nakiweka wakfu kwa.." "Nimekitoa kitabu hiki kwa…" (mhusika/wahusika hutajwa).

## 7. UHARIRI

Miongoni mwa kanuni muhimu za uandishi ni kuwa "Hakuna uandishi bora pasipo uhariri bora." Ni muhimu sana ukazingatia uhariri kwani utakuwezesha kufanya kazi bora ambayo itaonekana imefanywa kitaalamu. Zingatia mambo yafuatayo:

- Hakikisha unampa mtu mwingine ahariri kazi yako hata kama wewe ni mtaalamu wa uhariri.

- Hakikisha mhariri unayempa kazi yako ni mahiri katika lugha uliyotumia.

- Hakikisha mhariri anapata muda wa kutosha wa kuhariri hoja, mawazo, mpangilio pamoja na lugha katika kitabu chako.

- Baada ya uhariri ni vyema ukampatia mtu anayehakiki maandishi "proof reader" ili kuondoa makosa wakati wa kuandika na kuhariri "typing error"

## 8. MWONEKANO WA KITABU

Mwonekano wa nje wa kitabu hujumuisha jalada la nje "cover" pamoja na jina la kitabu. Eneo hili ni muhimu sana kwa kuwa linamsaidia msomaji kuamua anunue kitabu gani kati ya vingi sokoni. Zingatia:

- Jina la kitabu, kava na picha kwa pamoja hubeba dhana nzima ya kitabu. Hakikisha kuwa vinaakisi maudhui msingi ya kitabu na kumvutia mtu

kukichagua. Ni vyema kuchagua mtu mwenye taaluma ya kutengeneza makava ya vitabu akusaidie.

- Nyuma ya kava kunakuwa na maelezo mafupi kuhusu mwandishi wa kitabu na kuhusu maudhui ya msingi katika kitabu husika na namba za usajili wa kitabu (ISBN) na Bar Code.

## 9. USAJILI WA KITABU

Ili kulinda kazi yako unapaswa kuisajili katika mamlaka husika na kupewa hatimiliki ya kisheria. Vitabu vya kawaida vinasajiliwa kwenye Maktaba ya Taifa na vile vinavyotumika katika kazi za kisanii kama vile muziki, filamu nk husajiliwa na Baraza la Sanaa (BAKITA).